

NJIA YA MUNGU

ILIYOANDALIWA



Asante, Ndugu Sothmann.

Habari za asubuhi, marafiki. Ni, bila shaka tunayahesabu haya kuwa ni majaliwa makuu kurudi tena pamoja na jamii hii hapa Canada. Imekuwa muda tangu nilipokuwa hapa hapo awali, na daima nimetamani kurudi.

² Ninapenda watu wa mbuga pana na watu wa milimani, wao ni watu wa nyumbani tu, hakuna kitu, kile tunachokiita huko Marekani, ninii tu, “wa nyumbani,” watu halisi tu, ambaao unaninii tu, hamna ugumu wowote kuwahusu, wao ni watu tu wanaomtumainia Mungu, na kumwamini Mungu, na ni wanyenyekevu miyoni mwao. Na hivyo ndivyo Mungu anavyofanya kazi, akiwa na watu kama hao.

³ Haihitaji makusanyiko makubwa. Yesu kamwe hakuahidi kukusanyika pamoja na makusanyiko makubwa. Aliahidi kukusanyika kama ma..., uh, “Walipo wawili watatu wamekusanyika kwa Jina Langu, nitakuwa hapo katikati yao.” Na tena linasema, “Ikiwa watu wanaoitwa kwa Jina Langu watakusanyika pamoja na kuomba, basi nitasikia kutoka Mbunguni na kuiponya nchi yao.”

⁴ Na ni... Huu ni wakati mzuri sana. Kwa kweli nilikuwa nikija kwa likizo ndogo. Nimekuwa safarini sasa, sikuzote, miezi sita. Nayo hiyo mikutano ina *uharibifu* mkubwa kwa utu wangu. Nami nilihitaji mapumziko kidogo, nami nikawazia, “Vema, ama nitashuka niende pamoja na rafiki yangu, Ndugu Welch Evans, huko Florida, tukavue samaki kidogo,” ndipo ilitokeea nikawazia, “unajua, ingekuwa vizuri sana kama ningeenda huko Dawson Creek na kuvua samaki kwa muda kidogo, nikaenda kuwinda, nikamwona rafiki yangu Chris Berg, na baadhi ya ndugu huku.” Nikawazia, “Nisingekuwa ninamheshimu Mungu isipokuwa nifanye ibada kule kwa ajili ya watu.”

⁵ Kwa hiyo basi yote yaliishia kwa jambo moja, nami nikapitia mialiko yangu, nami nikaona mtu fulani alikuwa amechukua mahali pa Ndugu Hunter huko Dawson. Kwa hiyo nikampigia simu ndugu huyu, kwa kweli sijui jina lake, huenda akawa hapa asubuhi ya leo, nami nikaita...nikamwandikia barua. Naye akajibu na kusema, “Mbona, hakika tutaandaa mukutano mmoja ama miwili, ama siku moja ama mbili usiku, kwa ajili yako hapa.” Kisha kasema, “Nitakupa kiongozi ili uende ukavue samaki.”

⁶ Na—na kwa hiyo hilo lilinipa nafasi ya kuja kuwatembelea. Na kwa hiyo basi wakashuka wakaja, nikasema, “Vema, msisahau Grande Prairie, maana nitasimama hapo, labda wanawenza kunivumilia siku moja ama mbili, wakati nikiwa huko ndani.” Kwa hiyo hivyo ndivyo tuko hapa asubuhi ya leo.

⁷ Lakini tunakuja ku—kuwa baraka kwenu. Nami nina hakika mtakuwa baraka kwetu. Nasi tuko hapa, si kuwakilisha shirika lolote, tunajaribu tu kumwakilisha Kristo, na Yeye Ndiye. Nami nina hakika Yeye—Yeye... mnajmua Yeye kama Mwokozi wenu, ama ninatumaini mnajmua, katika msamaha wa dhambi zenu, na kujazwa na Roho.

⁸ Na sasa, mara nydingi mahali ninapoenda kuwaombea wagonjwa kote ulimwenguni, baadhi yao wanasema, “Ndugu Branham, mponyaji wa Kiungu.” Sasa, hilo ni kosa. Mimi si mponyaji, siamini mtu mwininge yejote ni mponyaji, ninaamini Mungu ndiye Mponyaji. Naye Mungu tayari amewafanyia yote yanayoweza kufanywa. Sasa, jambo linalofuata ni imani yako kuamini katika kazi Yake iliyokamilika.

⁹ Nami kamwe sikuja kuchukua mahali pa daktari. Mimi si daktari. Nami ni—ninakuja kuwaombea watoto wa Mungu, wagonjwa wa daktari, marafiki zangu. Na hiyo ndiyo sababu ya sisi kuwa hapa. Nasi tuna furaha kukutana katika kanisa hili dogo, jipya, zuri, lililo hapa juu katika—katika mbuga hii pana, watu wazuri.

¹⁰ Basi wakati tukija jana, niliona, ilinikumbusha juu ya, ama, wakati baba yangu alipokuwa akiniambia, huko chini katika jimbo la Kentucky, nilikozaliwa, walikuwa wakiingia na kukata miti na kuifingirisha, wanayaifingirisha magogo na kuyachoma moto, mwajua, basi wanaume wote wangechoma mahindi, nao wanawake wangetengeneza peremende, na kuifingirisha magogo, mwajua, na kuchukua, nadhani hayo yote ni mageni kwenu ninyi watu huku chini, na kula molasi ya mtama.

¹¹ Nilimwangalia jamaa mmoja kutoka Georgia, kwa namna fulani akatabasamu, anajua molasi ya mtama ni nini. Sijui ni wangapi hapa wanaojua molasi ya mtama ni nini? Kwani unatoka sehemu gani ya Kentucky, Dada? Naam. Vema, hakika naipenda. Nasi tulikuwa tukiengua mtama na kuwa na wakati mzuri sana.

¹² Sasa, na maskini, tulikotoka, maskini ile Baptisti ya Kimishenari ya Kusini, ambako tungekuwa na makusanyiko na kula chakula cha jioni humo, tuwe na Kutawadha miguu. Ni wangapi wanaojua Kutawadha Miguu ni nini? Kuninii Migu-..., loo, hilo lilikuja moja kwa moja kwenye kanisa la Kipentekoste. Tungekuwa na nyakati nzuri sana kule, yubile kuu.

¹³ Na sasa, tumekusanyika kuninii, sasa, kwa ajili ya yubile ya namna nyingine, yubile ya kiroho, ambapo sote tunayafahamu hayo mambo, na wema wa Mungu, na rehema Zake.

¹⁴ Ninakumbuka hapa, hapo awali, kulikuwa na watu wazuri. Huenda nikatamka vibaya hili—hili jina la Kinorwe au Kiswidi, chochote kile, mimi, inaonekana kwangu kana kwamba jina lao lilikuwa *Bonderud*, ama *Bonderud*, ama kitu fulani. Walinipeleka hapa nje kuwapiga risasi bukini fulani asubuhi moja. Nami nawaambia, fadhili zao zilikuwa nzuri sana, karibu ziniue.

¹⁵ Baada ya kumaliza ibada usiku huo, walikuwa na mlo mkubwa mno, vema, tunaoita huko Marekani, chakula cha jioni, nafikiri mnauita huku juu, chakula cha kutwa. Daima mi—mimi huchanganyikiwa katika jambo hilo. Kama—kama—kama hicho ni—ni chakula cha kutwa, basi nitakula chakula cha jioni lini? Mnaona, ni—ninachanganyikiwa kabisa na kukosa mlo mahali fulani kama hicho—ikiwa hicho, kama wakati wa jioni ndio chakula cha kutwa.

¹⁶ Sasa, huko chini Kusini, tunakiita kiamshakinywa chetu, chakula chetu cha kutwa, na chakula chetu cha jioni. Basi kama *hiki* ndicho chakula changu cha kutwa hapa *hatimaye*, basi imekuwa je kwa chakula changu cha kutwa? Mnaona, wapi, basi wapi, kama hiki ndicho chakula changu cha kutwa, basi chakula changu cha jioni kitakuja wapi? Kesho yake asubuhi, mnasema ni kiamshakinywa. Kwa hiyo silipati vizuri sana.

¹⁷ Kwa hiyo kwa vyovyote vile, nitalisema jinsi nilivyolija vizuri zaidi, nilikula milo miwili ya jioni. Nilikuwa na mmoja huko nje, ndipo nikalala kitandani yapata, loo, nadhani yapata saa saba, ama saa sita, na yapata saa kumi kesho yake wakaniamsha kwa ninii, kiamshakinywa changu. Nami nilikuwa huko nje kondeni, shamba dogo la shayiri, nikichimba shimo ili kutambaa niingie ndani, nipate kuwakwepa bata bukini. Ndipo basi, tukarudi yapata saa mbili baadaye. Mimi—mimi... Vyakula hivi vyote hapa vya jioni ambavyo nilivikosa hapa, vyote vililipiwa kule, maana nilirudi, nikala kiamshakinywa kingine, kwa hiyo nilikuwa na viwili siku hiyo, kwa hiyo nilikuwa ninii sana... Kamwe sitawasahau watu hao, natumaini nitapata kuwaona wakati nikiwa hapa.

¹⁸ Walikuwa na watu fulani huko Dawson Creek. Mmoja wao alikuwa ni mhudumu. Sijui, lakini ilionekana kwangu kama mimi... je, ninatamka jina hilo vizuri? *Bonderud*, *Bonderud*, *Bonderud*? Mmoja wao alikuwa ni mhudumu. Einar, naamini, ama Ined? Einar? Iver, Iver. Jamaa mkubwa mno, jamaa mzuri naye alikuwa... Aisee natumaini... Ati nini? [Ndugu fulani anasema, “Yuko kule, wa pili kule.”—Mh.] Iver Bonderud, vema, vema, huku mimi nikisimama hapa nikizungumza habari

zake, naye huyu hapa amesimama, akinisikiliza. Afadhali niache kuzungumza juu ya hayo, sasa hivi. Vema.

¹⁹ Baba na mama yako wameondoka, Ndugu Bonderud? Wote wawili. Kamwe siwasahau maskini hao Wanorwe. Nilikuwa nyumbani kwake, nyumba yake ya kasisi huko nje. Nami nilikuwa nikikaa huko kwa siku chache kwenye mahali padogo, Ground Birch. Hiyo ni kweli? Na maskini Mama na Baba Bonderud, maskini Wanorwe, mimi...hiyo ni kweli? Au Waswidi? Mmoja wa Waskandina..., Mnorwe. Huko juu nyumbani, na baba anashuka kwenda kumnunulia, uh, kununua vyakula kwenye duka dogo, naye mama alikuwa ameketi dirishani, mwajua, naye akaendelea kuvuta pazia, akimtazamia aje.

²⁰ Baada ya kitambo kidogo, huyu hapa akaja, mwendo wa kasi, mwajua. Naye a—alikuwa na ndoo ndogo mkononi mwake vifurushi vichache chini ya mkono wake. Ndipo mama akamwona akija, huyu hapa akaenda kumlaki, mwajua. Ndipo akachukua baadhi ya hivyo vifurushi na kumpigapiga mgongoni, mwajua. Nao hawa hapa wakaenda, wawili, maskini mume na mke wakija. Loo, niliuua tu mikono yangu na kulia, nikawaza, “Hiyo si ni nzuri?”

²¹ Ndipo kesho yake tukawa na yubile ya mlo, maana waliwaleta watoto wote, walikuwa na kila kitu kwa ajili ya chakula cha kutwa. Na hiyo ilikuwa saa sita, mwajua. Kwa hiyo tulikuwa na mlo mkubwa wa kutwa uliotandazwa huko nje.

²² Nami nilitaka kuzungumza sana na maskini hao mume na mke, na si—sidhani wangeweza kuzungumza neno moja la Kiingereza, wala nisingeweza kuzungumza neno moja la Kinorwe, kwa hiyo tusingeweza kuelewana tukiashiriana, mtu fulani alikuja na kunifasiria. Ndipo nikasema, “Unajua, moja ya siku hizi nitakapovuka mto, nikishuka kwenye mitaa ya Utukufuni, ninatarajia kumwona mwanamume wa Kinorwe mwenye sura nzuri na maskini mwanamke mrembo wa Kinorwe, kijana, asizeeke tena. Nami nitasema, ‘Hivi sikujui?’ Wanasesma, ‘Loo, naam, Ndugu Branham, unanijua, tulikulisha bukini mwitu siku moja mezani tulipokuwa huko chini duniani.’”

²³ Nami nasikia ya kwamba wote wawili wameenda kwenye Makao hayo ya Mbunguni. Mungu aziweke nafsi zao za thamani katika amani ndilo ombi langu.

²⁴ Sasa, asubuhi ya leo tumetoa nafasi, naye mchungaji ni mzuri sana kutupa wakati huu mdogo wa kujitambulisha, kwa namna fulani, kwa ibada. Na kwa kawaida sihubiri zaidi, ninapoenda kuhubiri, zaidi ya saa sita ama kitu kama hicho, kwa kawaida mimi huwaachilia, takriban, baada ya saa nne hadi sita za kuhubiri, karibu hivyo. Kwa hiyo wao... Lakini asubuhi ya leo tutachukua tu kama dakika thelathini za utangulizi tu,

halafu, hii, maana hamna budi kwenda nyumbani, na kula, kisha mrudi tena saa nane na nusu.

²⁵ Ni watu wangapi wanaotarajia kuombewa wakati huu wa mikutano? Hebu tuone mikono yenu, kote jengoni. Vema. Sasa, kama una watu wowote, kumbuka itakuwa upesi sana. Hatuna budi kuharakisha kuingia, kuharakisha kutoka. Tunakwenda Dawson. Na kwa hiyo, mnawapata hapa alasiri ya leo. Ibada itaanza saa nane na nusu?

²⁶ Loo, waleteni hapa kasorobo, kitu kama hicho, naye mwanangu, huko nyuma, atakuja kuwapa kadi za maombi, mtu yeoyote anayezitaka. Halafu hatutakuwa na, kama uwanja wa michezo, kila mtu atakuja tu wakati namba zao zitakapoitwa nasi tutawaombea hivyo.

Na sasa, kama una majirani wowote wanaotaka kuombewa, waleteni mapema alasiri ya leo wapate kadi ya maombi.

²⁷ Sasa, kabla hatujalikaribia Neno, hebu na tumkaribie Mwandishi wa Neno kwa njia ya maombi, huku tukiinamisha vichwa vyetu.

²⁸ Mungu mwenye rehema na Mtakatifu, tunakuja katika Uwepo Wako kwa njia ya maombi, katika Jina la Bwana Yesu, Mwana wa Mungu wa thamani na mtukufu. Kwa kuwa tumefundishwa katika Maandiko ya kwamba Yeye alitwambia kama tukiomba Baba lolote katika Jina Lake, litajaliwa.

²⁹ Sasa, kama tungekuja katika jina la kanisa hili la kupendeza, ama kwa jina la wachungaji, ama kwa jina la taifa, haingetufaa chochote, nasi tu—tusingekuwa na imani kwamba maombi yetu yangejibiwa. Lakini tunapokuja katika Jina hilo litoshelezalo kwa yote la Bwana Yesu, tuna hakikisho ya kwamba Mungu atatujalia kile tuombacho.

³⁰ Kwa hiyo tunayapima maombi yetu kuona kama tutaomba lolote bayo, kuona kama tuna nia mbaya ya kuja kwetu hapa, ama kuomba kwetu, ama nia tungekuja nayo katika kuomba mambo kama hayo. Kwa hiyo tunaomba, Mungu, ya kwamba Wewe uichunguze mioyo yetu, kwa kuwa tunasimama katika Uwepo Wako Mtakatifu katika maskani hii, tukijua ya kwamba sisi ni watu wanaolekea Umilele, huku vichwa vyetu vimeinamishwa kuelekeea mavumbini ambako Wewe umetutoa.

³¹ Nasi tunatumaini kwa uchaji ya kwamba siku moja utamtuma Yesu. Nasi tutainuliwa kutoka kwenye mwili huu wa mavumbini hadi kwenye mwili uliofanywa kama mwili Wake Mwenyewe wenye utukufu, ambako hakutakuwako na kuwaombea wagonjwa tena, hakutakuwako na mikutano ya maombi ya usiku kucha kwa ajili ya waliopotea, bali waliokombolewa watakuwa katika Mji huo nao watatembea katika Nuru yake milele. Loo, mioyo yetu inatamani jambo hilo.

³² Lakini wakati kungali mchana na tuna nafasi, tunakusihu Wewe, Bwana, kwa ajili ya uongozi na rehema Zako za Kiungu. Nasi tunatumaini ya kwamba utaupa mji huu mdogo uamsho mkuu wa uhalisi wa Kristo mionganoni mwetu hata leo, baada ya miaka elfu mbili tangu kusulubiwa Kwake, kwamba Yeye hajafa, bali Yu hai milele.

³³ Tunaomba, Bwana, ya kwamba utaruhusu Maandiko yatimie, ambayo yalinenwa kwa wanafunzi, uliposema, “Mnapoingia mjini, waponyeni wagonjwa walioko mjini.” Ninaomba, Bwana, ya kwamba wote wanaoteseka kwa dhambi, kwamba wataponywa kwanza, na halafu, hao wote, wanaoteseka kimwili wataponywa.

³⁴ Na jalia kuwe na uamsho mkubwa katika bonde hili dogo hapa, ambalo litasababisha njaa na kiu kubwa sana, kwa maana imeandikwa, “Ninyi ni chumvi ya dunia, na dunia ikipoteza ninii yake . . . , ama, chumvi ikipoteza ladha yake, tangu sasa haifai kitu, ila kutupwa chini ya miguu ya watu, na kukanyagiwa chini.” Lakini, Bwana, tunaomba ya kwamba utamjalia Kristo awe maishani mwetu kwa uhalisi *sana* hata watu watamwonea kiu. Jalia awe kiini cha mvuto, Bwana. Nasi tutakusifu Wewe kwa ajili yake katika unyenyekevu na kuinamisha vichwa vyetu kwa unyenyekevu, tukikupa Wewe sifa zote.

³⁵ Mbariki mchungaji hapa, na wachungaji washiriki, kila kanisa mjini na kote katika jamii, washiriki wote wa kila kanisa. Jalia tuje kwa moyo mmoja na nia moja na kuuona utukufu wa Bwana wetu aliyefufuka. Tunaomba hayo, katika Jina Lake, na kwa ajili ya utukufu Wake. Amina.

³⁶ Kwa njia tu ya—ya kutanguliza mikutano, ningetaka kusema ya kwamba tunakuja kila siku, kufanya tu kampeni ndogo. Maswali yoyote, unaweza kumwuliza Ndugu Sothmann, naye angweza kukuelekeza, ye ye pamoja na wachungaji.

³⁷ Na sasa, maswali juu ya maoni ya kidini, sijaribu kuyajibu kwa sababu huyo ndiye mchungaji, mnaona sisi, uh, afadhali kila kanisa lingefahamu, mchungaji wao ni mtu wa Mungu, aliawaongoza salama umbali huu, kwa hiyo anaweza kuwapeleka mbele, mnaona.

³⁸ Kwa hiyo sasa, njoni, mkiamini. Labda, pengine katika mkutano ujao au wowote ule, huenda kukawa na watu wa nje ambao—ambao wako nje ya milki za Kipentekoste na Full Gospel. Nasi tunataka kuwa na hakika, tukijua mahali tunaposimama, maana hakuna mtu anayeweza kutembea bila ya kuwa na hakika anajua anakotembelea. Mnaona? Tu—tunajua mahali tunaposimama, kwa sababu tunatembea pamoja na Maandiko, tukiamini ya kwamba Mungu hutimiza kila Neno na kulifanya halisi. Mnaona? Kama hamwamini hilo, basi hatuwezi—hatuwezi kutembea na Mungu.

³⁹ Na sasa, kila siku, kila mmoja, kabla ya kila ibada, hao wavulana watashuka na kusambaza, ama, Billy, kwa kawaida Leo na Gene, baadhi ya washiriki wa—wako kwenye miamsho mikubwa, nao wanasaidia kusambaza kadi pia, lakini mwanangu yuko wakati huu, naye atawapa kadi za maombi yapata saa moja kabla ya kila mkutano ili tusiwasumbue wa—watu wanaokuja kwa ajili ya, uh, kusikia ibada, mikutano ya utangulizi na kadhalika.

⁴⁰ Sasa, kama ninyi huweka kumbukumbu ya Maandiko ya yale, wakati mwingine, wahudumu wanasoma, ningependa kuwasomea kutoka katika Agano Jipy, Kitabu cha Yohana Mtakatifu, mlango wa 12 na kifungu cha 32, kwa ajili ya utangulizi, na kutokana na hili nataka kutoa fungu hili kwa ajili ya muktadha. Yesu alikuwa akizungumza. Loo, ningalipenda kumsikia akinena. Ninii tu, ninajua sisi sote tuna njaa ya jambo hilo.

Nami nikiinuliwa juu ya nchi, nitawavuta watu wote kwangu.

⁴¹ Sasa, tuna wimbo mdogo huko Marekani, tunauimba huo, *Nikiinuliwa Juu*. Sasa, ninataka kuzungumza juu ya somo la *Njia ya Mungu Iliyoandaliwa*. Mungu anayo njia iliyoandaliwa.

⁴² Sasa, mara kwa mara mwanadamu ulimwenguni hujaribu kufanya jambo fulani kufanikisha jambo fulani. Yeye ni, anataka kufanya hivyo mwenyewe. Mimi... Samahani kwamba imefanyizwa hivyo, lakini jamii ya binadamu iko hivyo tu. Mwanadamu hujaribu kufanya jambo fulani kujipatia mwenyewe mafanikio.

⁴³ Wakati nikija jana kwenye barabara kuu, nilipitia kwenye ile miji miwili mikubwa hapa chini, Calgary na—na Edmonton. Nami nilikuwa nikizungumza na mwanangu nilipoenda kununua petroli. Ndipo nilipoangalia pampu nayo ikasema, “Senti thelathini na tisa kwa galoni,” nikasema, “Sielewi jinsi wanavyofanya jambo hilo.”

⁴⁴ Petroli hii inatugharimu yapata senti thelathini na tano kwa galoni huko Marekani, nao wanaisafirisha hapa. Badala ya galoni ya kwati nne, wanawapa galoni ya kwata tano kwa senti thelathini na tisa. Kwa hiyo, wanaweza kuiuza huku juu sana mbugani, kwa bei nafuu kuliko unavyoiuza Marekani, na hata hivyo imetoka Marekani, ikaletwa huku juu. Serikali inainunua, halafu mtumiaji anaiuza, bila shaka, ndipo serikali inatoza kodi za hiyo kutoka kwa mtumiaji, inairudia serikali.

Ndipo Billy akaniambia, mimi, “Hivi hilo linaonekana ni haki, Baba?”

Nikasema, “Vema, tunaona kwamba wanaendelea vizuri kuliko sisi.”

⁴⁵ Sasa, kama mkiangalia, ninataka kusema hili kuhusu Canada. Ninaamini kama Yesu angekawia, kwa, tuseme, miaka hamsini, kwamba taifa hili litayaongoza mataifa ya ulimwengu. Hili litakuwa ndilo taifa mashuhuri sana la ulimwengu, Yesu akikawia. Kwa sababu ni serikali yenu iliyojisetiri, mnaona, na vi—vitu, rasilimali ambayo inawabidi kujengea.

⁴⁶ Sasa, mashamba yenu yamefunikwa na mafuta na madini, na—na milima yenu imejaa dhahabu, na fedha, na urani, na potashi, na kadhalika. Mna ninii, mna ukubwa wa karibu moja na theluthi mbili ya Marekani, Milki ya Canada.

⁴⁷ Hata hivyo mjini, ama, katika jimbo la New York, wana watu laki mbili na tisini na sita elfu zaidi katika jimbo la New York, kuliko Canada iliyo nayo katika Milki yote. Inawapasa, hapa, *kujimudu*, ila tu hamna watu wengi sana, na hiyo ni baraka, kwa maana wakati idadi ya watu, watu wanapoanza kukusanyika pamoja, dhambi inaingia.

Asubuhi ya leo tulipokuwa tukila kwenye kituo cha basi, mimi na mwanangu, alisema, “Baba, ningependa kuishi hapa.”

“Loo,” nikasema, “ni nani asingependa?” Mnaona? Hii ni paradiso. Labda hamtambui.

⁴⁸ Wengi, kama kina mama, wanatamani miji mikubwa, mara nyingi. Na *hiyo*, kamwe usitamani jambo *hilo*. Loo, jamani! Chukua *hii* wakati wowote. Hapa ndipo mahali pa kuwalelea watoto wako. Hapa ni mahali unapoweza kuwapatia mengi zaidi watoto wako, zaidi kwa watoto wako, zaidi kwako mwenyewe, kuliko mahali popote nipajupo.

⁴⁹ Pesa zenu zina thamani kubwa zaidi, au ya juu sana, kama si kubwa zaidi, kuliko taifa lingine lolote ulimwenguni. Kwa nini? Kwa sababu kwamba mnalima ngano yenu, serikali inaichukua na kuiuza kwa niaba yenu, na hizo pesa hazina budi kuwekwa, pesa taslimu.

⁵⁰ Sasa, huko Marekani, mkulima huikuza ngano, serikali inamlipa kutoka kwenye hazina ya serikali, kisha inazichukua, na kuyapa mataifa mengine nao kamwe hawalipi. Baadhi yao yamekuwa yakidaiwa kwa mamia ya miaka wala hawaii lipi kamwe. Nazo zinatoka kwenye mfuko wa serikali, ambalo linalifilisi taifa. Na hivi karibuni halina budi kuanguka, hivyo tu.

⁵¹ Na sasa, hatuna rasilimali tena; mna rasilimali nyingi sana, kwa sababu kama mimi na wewe ni... Ninakuuzia mchele badala ya ngano, lakini wakati nikiishiwa na mchele, basi nini? Mnaona?

⁵² Sasa, mna rasilimali, kwa hiyo ninyi, zaidi ya mahali popote ulimwenguni, kwa hiyo ninyi ni taifa linalokua, linalostawi. Nami nikasema, “Nina mvulana mdogo wa miaka mitano.” Nikasema, “Mwanamume Mkanada hapa, anaweza kusema,

kwa maskini mvulana wake mwenye umri wa miaka mitano, ‘Mwanangu, ninakulea hapa katika taifa ambalo kuna siku za usoni zenyе mafanikio makubwa kwa taifa hili.’’ Nikasema, basi, ‘Anaweza kumpa zaidi, mtoto wake katika mtazamo wa kitaifa, kuliko Mmarekani awezavyo, ama Marekani iwezavyo, kumpa mwana aliye huko chini, kwa sababu mna msingi zaidi hapa wa kurejea, kitu ambacho kina matumaini makubwa,’’ na kadhalika.

⁵³ Sasa, lakini kama Urusi kamwe ikija Marekani, ambayo ni moja ya mataifa yanayoongoza katika ulimwengu wa magharibi, wasingetaka kuilipua, wangeweza kufanya hivyo, kama wangetaka, sasa hivi, la sivyo tungeweza kuilipua *hiyo*. Lakini kamwe hawatafanya hivyo, kwa sababu wangeangamiza kila kitu, wanataka utajiri wa hili taifa, kwa hiyo basi, watajaribu kuwafanya walale.

⁵⁴ Na jambo moja, sidhani vita hivyo vitakuwa ni vita vya makombora. Lakini nafikiri vitakuwa ni vita vya kiroho, ambavyo vitaingia na kuliteka tu hili taifa na kuwalaza usingizi, mpaka watakapoingia na kulishikilia. Vema, wakishikilia kule na kuiteka Marekani, Canada ni kitu kidogo kwao.

⁵⁵ Kwa hiyo basi, kweli hakuna kitu ulimwenguni ambacho tunaweza kujengea matumaini yetu, mnaona, juu ya mafanikio yoyote ambayo tungeweza kutoa katika ulimwengu huu, kwa sababu hakuna matumaini kwake. Kuna Tumaini moja tu, hilo ni Kristo, ni kweli.

⁵⁶ Kwa sababu, pipi kama sayansi leo hii, inajaribu kujenga kitu fulani? Bo-bo-bomu litakalopaa juu sana ama ninii fulani... wamweke mtu katika sputniki na kumtuma juu angani. Urusi ilijivuna, hivi majuzi, ulimwenguni kote, walikuwa na mtu angani, wakamweka mtu juu angani.

⁵⁷ Vema, hilo si jambo la kujivunia. Tulikuwa na Mtu angani kwa miaka elfu mbili: Yesu Kristo. Sio kupanda tu kidogo *huku* juu na kurudi, bali kote kote Utukufuni na kurudi pamoja na majeshi ya Malaika kutuhudumia. Kwa hiyo tumekuwa na Mtu angani kwa muda mrefu, Urusi haitushindi kwa chochote. Mtu huyo alirudi kukaa, Yesu anaweza kwenda popote atakapo.

⁵⁸ Kwa hiyo sisi ni... tunaweza kusema hivi: Vipi kama leo, sasa, ndugu zangu, dada zangu Wakanada, pipi kama leo hii, kwamba sayansi ingeweza kukamilisha kitu ambacho kingeweza kuweka kifaa kidogo mwishoni mwa shamba la mtu, na wangeweza kukifungulia, na mvua, kuleta mvua kutoka angani, au kuikomesha, kulifanya jua liangaze, chochote ulichohitaji? Hayo yangekuwa ni mafanikio! Loo, jamani!

⁵⁹ Vipi kama tulikuwa na kitu ambacho wangeweza kusema wangeweza kumfanya m-mtu ambaye—ambaye anakufa kwa kansa, arudi na kuwa mzima tena? Hayo si yangekuwa ni

mafanikio! Kama vile chanjo ya Salk kwa watoto, ilienea ulimwenguni kote.

⁶⁰ Lakini tuseme, kwa mfano, vipi kama sayansi ilikuwa imepata kitu fulani, dawa ndogo ambayo wangeweza kuitia kwenye kijiko, na wangeweza kuimimina kwenye kinywa cha mzee, ama mwanamke mkongwe, mwenye umri wa miaka tisini, na kuiangalia kwa yapata, huyo mgonjwa, kwa yapata dakika moja, na kuwaona wakirudi kuwa kijana mwanamume na mwanamke, akiwa na damu ambayo kamwe isingezeeka, na kiumbe ambacho hakitakufa kamwe? Mbona, filimbi zingelia, mataifa yangepiga mayowe, “Mauti yalikuwa yamekwisha, hakuna uzee tena, hakuna mauti tena, tumeyashinda.” Mbona, kingekuwa ni kitu kizuri mno!

⁶¹ Watu wanajaribu kupata hilo kuptitia rasilimali ya, vema, ya fasihi, au utamaduni, elimu, sayansi. Ni kitu gani kinachowafanya watafute hayo? Ni kwa sababu hicho kipo mahali fulani, hiyo ndiyo sababu wanakionea njaa. Kama Daudi alivyosema, “Kilindi kinapoita kilindi,” kabla hapajakuwa na kilindi kinachoita, hapana budi kuwe na kilindi cha kuitikia wito huo.

⁶² Kabla hapajakuwapo na pezi mgongoni mwa samaki, ilibidi kuwe na maji apate kuogelea kwanza, la sivyo asingekuwa na pezi. Kabla hapajakuwapo na m—mti wa kukulia ardhini, ilibidi kuwe na ardhi kwanza, la sivyo kusingekuwako na mti.

⁶³ Kama ambavyo nimesema mara nydingi, nikinukuu hili, wakati fulani uliopita, huko Marekani, mvulana mdogo alipatikana shu—shuleni, akila vifutio kutoka kwenye penseli zake. Kisha mama yake akamkuta nje kwenye ukumbi wa nyuma, akila pedali kutoka kwenye baiskeli, pedali ya mpira. Basi wakampeleka maskini jamaa huyo kwenye kliniki akachunguzwe, ndipo walipofanya hivyo, walikuta kwamba maskini mwili wake ulihitaji salfa. Kwa hiyo basi, salfa iko katika mpira, na hapo, alipokuwa akila mpira, alikuwa akiridhisha shauku hiyo ya salfa.

⁶⁴ Lakini loo, hebu niseme hivi: Kabla hapajakuwapo na shauku ya salfa mle ndani, ilibidi kuwe na salfa mahali fulani kuitikia shauku hiyo.

⁶⁵ Na wakati kukiwa na shauku katika moyo wa mwanadamu kupata mahali pa amani, kupata mahali pa ukamilifu, kuupata uzima, kupata mahali penyewe, chemchemi ya ujana, ambapo wazee wanaogelea mle wakarudi wakiwa vijana tena, hapana budi pawe na mahali hapo kwanza, la sivyo jamii ya binadamu isingepatamani.

⁶⁶ Tumekusanyika hapa katika mkutano huu mdogo kuzungumza juu ya uponyaji wa Kiungu. Hapana budi kuwe na Chemchemi iliyofunguliwa mahali fulani la sivyo kamwe hungeitamani. Kuna kitu fulani miyoni mwenu asubuhi ya leo,

ninyi watu, kinachowaambia kuna Mungu anayeweza kuponya. Na kwa hakika kadiri shauku hiyo ilivyo moyoni mwako, hapana budi kuwe na Chemchemi mahali fulani kuridhisha shauku hiyo, la sivyo kamwe usingekuwa na shauku hiyo.

⁶⁷ Kwa maneno mengine, kabla hapajakuwapo na kiumbe, hapana budi kuwe na Muumba kuumba hicho kiumbe moyoni mwako. Natumaini hilo linaleta maana, Muumba kuumba kiumbe. Kwa hiyo kiumbe hakina budi kuweko kwanza na kisha Muumba wa kukionea shauku.

⁶⁸ Sasa, mwanadamu amejaribu kupata jambo hili kupitia sayansi, lakini inaonyesha ya kwamba lipo. Sasa, kwa nini mwanadamu asiachane tu nalo? Nao huchimba chini ardhini wapate visukuku ili kukanusha jambo fulani na kuthibitisha jambo fulani. Wanachukua na kushika atomi za hewani na kuzivunja na kuchukua molekuli na kadhalika wakijaribu ku—kuthibitisha jambo fulani.

⁶⁹ Wanachukua makombora yaya haya, na kila wanapojaribu kuumba kitu fulani kwa njia ya sayansi, anajiangamiza mwenyewe, linamsukumia mbali zaidi na Mungu wakati wote. Badala ya kukaribia hayo mafanikio, ye ye hujisukumia mbali na hayo mafanikio.

⁷⁰ Wakati alipovumbua baruti, anamwua ndugu yake. Wakati alipovumbua motokaa, sayansi, alifanya nini? Inaua kuliko baruti. Sasa, mwenyewe ana bomu la atomiki, bomu la haidrojeni. Mnaona, anajipeleka mbali zaidi na Mungu.

⁷¹ Katika bustani ya Edeni kulikuwa na miti miwili, mmojawapo ulikuwa ni Mti wa Uzima, huo mwingine mti wa mauti, uh, ule mti wa maarifa. Na wakati mwanadamu alipouacha Mti wa Uzima apate kula kutoka kwenye mti wa maarifa, kuuma kwa kwanza alikouma, alijitenga na Mwumba wake.

⁷² Na kila wakati anapouuma mti huo wa sayansi na maarifa, anajiuua, anajipeleka mbali zaidi. Kwa nini asirudi tu kwenye huo Mti? Hilo ndilo suluhisho pekee, airudie hali aliyouumbiwa na Mungu kwa mara ya kwanza.

⁷³ Sasa, mwanadamu amejaribu kufanikiwa hata hivyo, wakati wote. Sasa tunawazia juu ya Nimrodi, wakati anapowazia juu ya wakati mmoja ambapo Mungu aliuangamiza ulimwengu kwa maji, huyu mtawala mkuu wa Babeli, alisema, "Ninaweza kupita na hiyo." Mnaona, ye ye anajaribu kupata kitu fulani, ni asili yake, mwanadamu hufanya hivyo.

⁷⁴ Alithibitisha asili yake wakati Adamu alipouuma ule mti wa maarifa, akajitenga na Mungu, alijaribu kujifanya njia ya kumrudia Mungu kwa kujifunika kwa majani ya mtini, dini, akijifanya mwenyewe, alikuwa akijaribu kufanya wokovu bila ya upatanisho.

⁷⁵ Nasi tunaona mtu huyo, angali anafanya jambo lile lile siku hizi, akijiunga na kanisa, akiandika jina lake kwenye kitabu, akijaribu kutafuta njia ya—ya kukariri sala chache kwa njia fulani, au kurudia kanuni kadhaa za imani, akijaribu kupata wokovu bila upatanisho. Huwezi, huna budi kuwa na upatanisho kwa ajili ya dhambi. Nayo dhambi ni kutokuamini, hakuna dhambi nydingine ila kutokuamini.

⁷⁶ Mara nydingi nimesema ya kwamba kunywa pombe, kufanya uzinzi, na kuapa si dhambi, hizo ni sifa za dhambi, wewe ni asiyeamini, sababu ya kufanya hivyo. Lakini kama kweli ulimwamini Mungu, usingeefanya hivyo. Mnaona? Usingeewenza kufanya hivyo, kama wewe ni mwaminio.

⁷⁷ Sasa, tunaona basi ya kwamba mwanadamu amejitenga na Mungu na daima akijaribu kutumia mti uo huo wa maarifa kurudi, huku akijipeleka mbali zaidi, wakati wote.

⁷⁸ Kwa hiyo tunaona Nimrodi, mara baadaye alijaribu kujijengea mnara, mnara wa kidini, kwamba kama Mungu kweli aliuangamiza ulimwengu tena, angefanya nini? Angepanda juu, na kuwachukua watu wake, na kupanda juu ya mafuriko, juu kwenye—juu kwenye ule—ule mnara, naye angepanda juu yake. Iliishia wapi, ilikuwaje? Katika mafanikio yake yote, ajifanyie jina kuu, aliangamia pamoja na mnara wake.

⁷⁹ Baadaye, kulikuwa na mtu jina lake mfalme Nebkadreza. Naye alifikiri angeweza kujenga mji, aiweke sayansi mle ndani, wafanyakazi wake mashuhuri. Naye angefanya nini? Alijenga ukuta kuuzunguka mji huu fulani unoaitwa Babeli, ambao wangeweza kufanya mashindano ya magari ya farasi juu yake. Yale malango, nafikiri yalikuwa na upana wa futi sabini. Nao walikuwa wakubwa sana hata ilichukua karibu kundi la askari kulifungua lango. Hakuna mtu angaliweza kulikaribia hilo.

⁸⁰ Na mara tu anapofikiri amefanikisha kitu fulani, ye ye hujizamisha tu kiasi *hicho* katika dhambi.

⁸¹ Na wakati kanisa linapoanza kuwazia, kwamba, “Kwa sababu sisi ni *hiki-na-hiki*, sisi ndio kanisa kuu, sisi ndio kanisa kuu,” wanawaachilia watu wao kufanya dhambi, kutokuamini, “Siku za miujiza zimepita, hatuzihitaji hizo tena.”

⁸² Mara tu anapowazia ya kwamba amefanya jambo fulani, amepata mafanikio, badala ya kuja na kuchukua njia ilioandaliwa na Mungu kwa ajili yake, ye ye hujaribu kujitafutia njia mwenyewe, kitu ambacho anaweza kusema, “Nimefanya jambo fulani.” Mwanadamu hawezi kuokolewa kwa jambo moja analofanya. Wokovu ni kwa neema, si kwa matendo, bali kwa neema, ni kitu ambacho Mungu anakupa.

⁸³ Sasa, tunaona ya kwamba Nebkadreza, mara alipoona ya kwamba alikuwa amepata mafanikio makubwa, alitoka nje kwenye baraza lake siku moja na kusema, “Angalieni yale

ambayo nimefanya,” ndipo Mungu akaubadilisha moyo wake na kumfanya mnyama kondeni.

⁸⁴ Mjukuu wake akaja, juu ya, Belshaza, ambaye alikuwa mjukuu wa Nebkadreza, naye akachukua kutoka kwa kile babu yake, lile dhehebu kuu, ama chochote kile, ambacho babu yake alitegenezza, naye alikuwa anaishi kwa anasa nacho.

⁸⁵ Ambayo mengi ya makanisa yetu siku hizi, juu ya msingi wa wale watengenezaji wakuu hapo mwanzo yameunda kanisa, nasi tunajaribu kuingia tu katika mambo ya kijamii, badala ya mpango wa wokovu, katika kusema, “Sisi—sisi ni wafuasi wa kanisa *fulani-fulani*, sisi ni washiriki wa kanisa *fulani-fulani*.” Hilo halina uhusiano wowote na wokovu.

⁸⁶ Wokovu ni kuzaliwa upya ambako huja kwa Damu ya Yesu Kristo ambayo hutusafisha na kutokuamini kwote na kututenganisha kama watu wa kipekee kwa Mungu. Wokovu, si kitu tulichofanikisha. Nasi tunajifanya tu, vema, tunajipumbaza tu, tukifikiri ya kwamba tungeweza kufanya hivyo.

⁸⁷ Sasa, angalieni, wakati Belshaza alipofikiri alikuwa na kila kitu chini ya mamlaka yake, ndipo alianza kudhihaki vitu vitakatifu vyta Mwenyezi Mungu. Alichukua baadhi ya vyombo vilivytakaswa na kuanza kuvinywea divai, na kufanya, kufanya mizaha kuhusu baadhi ya ninii yetu...kama baadhi ya siku zetu za kisasa leo, kuyadhihaki mambo matakatifu ya Mungu. Unasema, “Hao ni kundi la watakatifu wanaojibingirisha, ha—hawajui wanaloafanya, wao ni *hivi-na-hivi*.”

⁸⁸ Mwajua, karibu tuwe na karamu ya aina ile ile ya Belshaza ulimwenguni leo? Kuwadhihaki watu, kusema, “Hao ni walokole, wendawazimu wa kidini, tusingejihuisha nao.”

Walidhani walikuwa salama nyuma ya ukuta huu. Lakini mnajua, Mungu anaweza kuangalia chini kutoka Juu.

Natumaini siwazibi maskio ninyi watu, nikiwapigia kelele, kwa sababu nimezoea kuzungumza katika kumbi kubwa za mikutano. Nitapunguza kidogo. Mnaona?

⁸⁹ Sasa, wakati anapodhania ana kitu fulani, ndipo Mungu anashuka na kuharibu jumba lake la michezo, kama alivyofanya la Belshaza.

⁹⁰ Nchi yetu tunayoipenda ya Marekani, tulidhani tungeweza kufanikisha jambo fulani, tukiwa mzao wa Uingereza, kutoka kwa malkia wa baharini. Tunafanya nini? Tuliunda meli, nasi tukasema, “Meli hiyo haiwezi kuzamishwa,” iliitwa Titaniki. Tulifikiri tulikuwa tumefanya jambo fulani, tulikuwa tumefanikisha jambo katika maisha ya baharini, ambalo hakuna mtu angaliweza kuweka mkono wake juu ya hiyo, tulikuwa tumefanya jambo fulani. Lakini katika safari yake ya baharini, Mungu kwa mkono Wake wenye nguvu, alionyesha ya kwamba

kile mwanadamu anachojaribu kufanya kitazama na kushindwa, akaizamisha.

⁹¹ Wafaransa, kwenye ile ngome ya Maginot, walidhani kusingekuwako na vita tena baada ya Vita vya Kwanza vya Dunia. Baada ya Canada, na Marekani, na kadhalika, walipovuka na kuwasukuma Wajerumani nyuma, wakajenga ngome ya Siegfried, basi walipofanya hivyo, ninaamini iliitwa ngome ya Maginot, wa-wakazizima bunduki, wakiukabili Rhine, wakaingia Ujerumani, na kusema, "Ujerumani ikiwahi kutushambulia tena, tumeimarishwa na ngome." Lakini Adolf Hitler akazunguka moja kwa moja nyuma yao, akaiteka.

⁹² Walifanya nini? Walijaribu kuishi katika dhambi, wanawake, divai, na anasa. Mungu hadhifikasi, msidanganyike, Mungu hadhifikasi, chochote apandacho mtu, ama taifa, ndicho watakachovuna, kwa watu binafsi au kwa mataifa.

⁹³ Nasi hatuna budi kukumbuka hilo. Tunapoamini kwa moyo wetu wote, kwamba Mungu anatutembelea sasa katika tukio maalum la kukusanyika hapa katika Grande Prairie, kumbukeni hilo. Mungu hafanyi lolote kwa ajili ya hadithi za kubuniwa tu, Yeye ana kusudi katika kufanya mambo haya, Yeye ana jambo fulani niani Mwake ambalo anajaribu kufanya. Tunaweza tu kupata kile anachofanya, kupata kujua mapenzi Yake, ingetulazimu kuchukua muda kidogo na kuomba, tuone kile Baba yetu anachojaribu kufanya.

⁹⁴ Sasa, tunaona basi, mara baada ya hiyo ngome ya Siegfried, ama, ngome ya Maginot, Wajerumani basi wakajijengea ngome nyingine. Ninaamini iliitwa Siegfried, mojawapo, huenda ikawa vinginevyo. Lakini wao walisema, "Tu—tu—tutajijengea ngome humu ndani na kuweka nyenzo ze—ze—zetu zote hapa chini."

⁹⁵ Na—nao Wajerumani wa thamani walikuwa wamemkubali Adolf Hitler, yule kiongozi wa mabavu, na, uaminifu, waliokuwa wameweka juu ya mtu huyo. Ndio kwanza niondoke Ujerumani hivi majuzi, yote Ujerumani inayohitaji ni uongozi, nami nikasema, "Angalieni kile mllichofanya kwa kuweka imani yenu juu ya kiongozi wa mabavu. Baba yuko huko juu kabisa upande mmoja wa hilo eneo, naye mama hapa chini, naye dada akifanya kazi mahali pengine, na ndugu ameuawa, basi angalieni mahali mlipofikia. Ninyi ni watu wazuri, lakini mliweka imani yenu kwa mtu asiyefaa. Chukueni uaminifu huo na muuweke juu ya Yesu Kristo ndipo mwone mahali mtakapotokea." Watu wazuri, lakini wakiweka uaminifu wao mahali pabaya.

⁹⁶ Hebu tusipatikane na hatia ya jambo hilo. Na tuweke uaminifu wetu juu ya Yesu Kristo. Kama vile Eddie Perronet alivyoshangilia katika saa yake:

Nyote zisifuni nguvu za Jina la Yesu!
Malaika na wasujudu;

Leteni taji ya kifalme,
Na kumtawaza kuwa Bwana wa wote.

Haya basi.

Kwa kuwa juu ya Kristo, Mwamba imara
ninasimama;
Sakafu zingine zote ni mchanga udidimiao.
Mataifa yanavunjika, Israeli inaamka,
[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]
Ishara ambazo manabii walitabiri;
Siku za Mataifa zimehesabiwa, zimekumbwa
na hofu;
“Rudini, Enyi mliotawanyika, makwenu.”

⁹⁷ Tuko katika wakati wa mwisho. Hebu tuyatafute mapenzi ya Baba yetu, tufanye kazi ya Baba yetu, tukijaribu kutojifanyia wenyewe jina.

⁹⁸ Tunaona jambo hilo mionganoni mwa wainjilisti, wainjilisti wakubwa, wakati mwingine wanajisikia wao ni wakubwa sana hawawezi kuja kwenye makanisa madogo na kadhalika. Jina kubwa! Kuna Jina moja tu kubwa mionganoni mwa Wakristo, hilo ni Jina la Yesu Kristo, ambalo kila goti litapigwa na kila ulimi utakiri siku moja. Hilo ndilo Jina kuu mionganoni mwetu: Yesu Kristo.

⁹⁹ Lakini tunaona, Titaniki yetu ilizama, Ngome ya Hitler ya Maginot, ama ile ngome ya Siegfried, haidhuru ilikuwa ipi, ilipondwapondwa vipande-vipande. Tunajikuta kuwa nini basi? Mwishoni mwa barabara. Mafanikio yetu si mazuri, kwa hiyo kwa nini kujipumbaza nayo? Hebu tuone kama Mungu anayo njia na mafanikio.

¹⁰⁰ Wakati Mungu alipokuwa anaenda kuuangamiza ulimwengu, wakati mmoja, kwa sababu ya dhambi na uovu wake, Nuhu alimjengea Mungu safina.

¹⁰¹ Hatutaki kujaribu kufanikisha chochote, kwa sababu hakuna kitu kwetu cha kufanikisha kwa njia hii, tunakubali tu kile ambacho tayari kimefanikishwa.

¹⁰² Mungu alimfanya Nuhu kujenga safina ambayo ingeuokoa ulimwengu, kama wangali amini jambo hilo. Lakini Mungu alijua hawataokolewa, kwa hiyo aliifanya urefu wa dhira *nyingi* sana.

¹⁰³ Kama alivyofanya katika siku za Nuhu, Yeye aliahidi kufanya wakati wa kuja kwa Mwana wa Adamu. Yeye ana Injili, haiwafikii na kuwaruhusu wanaume na wanawake waingie katika Ufalme wa Mungu wamejaa dhambi na kutokuamini, ni nyembamba, bali ndiyo njia. Alijua ni nani angeingia, bali ni njia Yake ilioandaliwa.

¹⁰⁴ Wote waliomsikia Nuhu, akisimama katika mlango huo na kuhubiri hukumu... Wakati mwingine linasikika

la kimapinduzi, na daima limekuwa hivyo, kwa moyo usioamini, lakini kutokuamini hakumzui Mungu, kutokuamini humsimamisha tu asiyeamini. Hakukomeshi... Huwezi kulizuia jua kuangaza kwa kutokuamini, wala usingeweza kusimamisha mpango wa Mungu kwa kutokuamini kwako.

¹⁰⁵ Yohana Mbatizaji alisema, "Mungu anaweza katika mawe haya kumwinulia Ibrahim watoto." Mnaona? Neno la Mungu limenena, halina budi kutimia. Mnaona? Mtu fulani atalisikia, mtu fulani atapata manufaa Yake. Sisi sote tuna hiari ya kujichagulia, tunaweza kujichagulia.

¹⁰⁶ Lakini angalia, ni kitu gani kilichotukia katika siku za Nuhu? Wote waliosikia waliitwa walokole, walimdhihaki huko juu kilimani, akijenga hii safina, wala maji hayajashuka kamwe, ndipo huenda sayansi ilimjia na kusema, "Kwani maji yako wapi? Nionyeshe mahali yalipo."

¹⁰⁷ Lakini mpango wa Mungu kamwe haujawahi kuwa juu ya mambo ya kimwili, umekuwa ni imani katika Neno Lake. Hiyo ndiyo njia ya Mungu iliyoandalishi, kuliamini Neno Lake kwa ajili yake, kuliamini, jambo ambalo huwezi kuthibitisha kisayansi.

¹⁰⁸ Nuhu akasema, "Siwezi kuwaambia hayo maji yako wapi, lakini Mungu aliniambia yatakuja, hilo ni zuri vya kutosha kwangu." Kwa hiyo akijenga safina, akajiweka tayari kwa ajili yake.

¹⁰⁹ Wakati Israeli walipokuwa utumwani huko chini Misri, kulikuwako na mtu jina lake Musa, siku moja, aliyekuwa akichunga kondoo, nabii mtoro, nyuma ya jangwa, naye akaona kichaka kikiwaka moto. Naye akapanda na mambo yote ya kiakili ambayo angeweza kupewa, angeweza kuwafundisha Wamisri hekima. Mungu alikuwa amemwita arudi huko chini, ambako alikuwa ameshindwa, na katika kujaribu kufanikisha kwa nafsi yake mwenyewe, akamwua Mmisri, akawazia, "Hakika, mimi ndiye jamaa huyo." Lakini mnaona, tunapoingia katika njia yetu wenyewe, tukijaribu kufanya lolote kwa njia yetu wenyewe, tuko nje ya mpango wa Mungu.

¹¹⁰ Hatuna budi kulichukua Neno Lake na kudumu moja kwa moja Nalo, kama tunaweza kuliona au la, kama linaonekana ni la kweli ama si kweli, dumuni na Neno Lake. Ni jambo ambalo tayari limefanikiwa, kwa sababu Mungu hana kikomo, Yeye hawezi kushindwa. Haidhuru linaonekana la kigeni jinsi gani, na jinsi linavyoonekana lisilo halisi, halina budi kuwa halisi, kwa sababu Yeye ni—Yeye yuko kila mahali, anajua yote, hana kikomo, Naye... kila Neno ni kamilifu.

¹¹¹ Hawezi kubadilisha mpango Wake, ningeweza kubadilisha wangu, unaweza kubadilisha wako. Ninaweza kusema jambo fulani, ikanibidi kulighairi, mimi ni mwanamume, wewe ni mwanamume na mwanamke. Lakini Mungu akiwa hana kikomo,

hawezi kufanya uamuzi mwingine kulihusu, hana budi kudumu na uamuzi Wake wa kwanza, kwa sababu kila uamuzi ni mkamilifu.

¹¹² Mnaona, tuna kikomo, tunaweza kusema, “Vema, ni—ni—nilikosea.” Lakini Yeye hawezi kukosea na awe ni Mungu. Kwa hiyo ile hatua aliyochukua juu ya...kama aliiwtwa jukwaani wakati mmoja kumwokoa mwanadamu, naye akamwokoa mtu huyo kwa msingi fulani, kama mtu yeoyote, wakati wowote, mahali popote, akikutana kwenye msingi uo huo, Mungu anawajibika kufanya hivyo tena.

¹¹³ Kama alimponya mtu kwa sababu ya imani yake, itambidi kutimiza hali iyo hiyo kila wakati, ama alikosea wakati alipomwokoa mtu wa kwanza, ama alipomponya mtu wa kwanza. Mnaona? Hilo ndilo alilotufanikishia: Imani! Imani ya kuamini Neno Lake!

¹¹⁴ Sasa na—naweza kusema jambo hili, katika kufunga, Musa asingeweza kuyachuna hayo majani kutoka kwenye mti na akaenda kwenye maabara yafanyiwe uchunguzi kuona ni kwa nini hayakuteketea, kama ingalikuwa hivyo, alishangaa mti huo ulinyunyiziwa nini, yeye mwenyewe alikuwa mwanasayansi.

¹¹⁵ Wanasayansi wa Kimisri walikuwa mbali sana na wa kwetu sasa, tumeninii... daima wamekuwa hivyo, moja kwa moja hadi wakati huu. Walijenga sfinksi na piramidi na kadhalika ambazo hatuwezi kuzijenga sasa, lakini, walikuwa na rangi, wangweza kuitia kwenye nguo za maiti zao, hizo zingali zinashikilia rangi yake kwa maelfu ya miaka, hatuna kitu kama hicho, mnaona. Sasa, lakini walikuwa wameendelea katika sayansi.

¹¹⁶ Lakini Musa kamwe hakujaribu kupata sababu kwa uchunguzi wa kisayansi, aliamini tu Neno la Mungu.

¹¹⁷ Hiyo ndiyo sababu tuko hapa katika Grande Prairie. Hiyo ndiyo sababu ya kanisa hili kusimama hapa asubuhi ya leo. Si juu ya dini yetu kujaribu kuthibitisha kisayansi ya kwamba tunaweza kuyafanya macho ya vipofu yafunguke, au kuyafungua masikio ya viziwi. Ni kuliamini Neno la Mungu. Ni kusema jambo lile lile alilosema Mungu, jambo ambalo limetimizwa kwa ajili yetu nasi tunaliamini. Haitubidi kuliwazia, Mungu aliliwazia.

¹¹⁸ Siwezi kuwaambia ni kwa nini ng’ombe mweusi anaweza kula nyasi ya kijani kibichi, na kutoa maziwa meupe, bali yeye hufanya hivyo. Mnaona, siwezi kujua mambo hayo, sijui, bali ninafurahia maziwi.

¹¹⁹ Siwezi kuelewa ni jinsi gani mwenye dhambi ambaye amezama *sana* katika dhambi, aibu *sana* hata mbwa asingemtazama ka—kahaba mtaani, jinsi ambavyo Damu ya Yesu Kristo inaweza kumfanya huyo kuwa mama wa heshima. Siwezi kuelewa jambo hilo, ninalikubali, Yeye analifanya.

Nisingeweza kuelewa ni kwa nini mimi, kipofu!

Nisingeweza kuelewa jinsi Mbunge Upshaw, kiwete kwa miaka hiyo yote!

¹²⁰ Florence Nightingale, wa Uingereza, marehemu Florence Nightingale, yule, vema, yule, si marehemu Flor- . . . , mjukuu, kitukuu wake, huku akiliwa na kansa! Labda mna kitabu changu chenyé hiyo picha ndani yake, hakuwa na uzito wa ratili sitini, naye ni mwanamke mwenye afya, mwenye nguvu. Siwezi kuelezea hilo, wakati wataalamu wa juu wa matibabu wa Uingereza na Afrika walikuwa wamemsusa afe, naye anaishi leo. Siwezi kulielezea hilo, ndugu, sijaribu kulielezea, ninaliamini tu.

¹²¹ Siwezi kutunga jambo fulani kwa ajili ya mafanikio yangu binafsi. Nami siwezi kuja hapa na kuwaambia na kuwaelezea uponyaji wa Kiungu; hakuna mwингine anayeweza. Lakini nimekuja hapa kuunganisha imani yangu na yenu kuamini katika kitu Fulani ambacho tumefanikishiwa, huyo ni Yesu Kristo Mwana wa Mungu, Yeye aliyefanikisha hilo kwa ajili yetu pale Kalvari.

¹²² Nuhu alikuwa na safina. Musa alikuwa na fimbo mkononi mwake ya kufanikisha jambo hilo. Ilikuwa ni Neno la Mungu. Safina hiyo ingeleeaje wakati vitu vingine havingeelea? Nisingeweza kuwaambia. Mungu alisema hivyo. Musa alikuwa na fimbo mkononi mwake. Fimbo hiyo ilikuwa nini zaidi ya fimbo nydingine yoyote? Lakini ilifanya nini? Ilifunga kinywa cha wasioamini, ilifunga Bahari ya Shamu, ilileta maji wakati wa kiu, na chakula wakati wa njaa. Ilikuwa ni kitu gani? Mungu alikuwa ameyafanikisha kwa fimbo hiyo.

¹²³ Wale mamajusi, walikuwa na nyota, na kwa nyota hiyo, walifuata mafanikio ya Mungu. Safina ilikuwa ndiyo mafanikio ya Mungu katika siku hiyo. Fimbo ilikuwa ndiyo mafanikio katika siku za Musa. Ile nyota ilikuwa ndiyo mafanikio katika siku za mamajusi.

¹²⁴ Ndugu, dada, marafiki Wakanada, Kristo ndiye Mafanikio ya Mungu kwa ajili yetu leo, kwa kufufuka katika wafu, na kumleta mbele zetu, kwamba Yeye hajafa, Yeye yu hai milele. Na Yeye yuko hapa sasa mionganoni mwetu alasiri ya leo, katikati yetu sasa, apate kujionyesha Mwenyewe akiwa hai.

¹²⁵ Si kile ninachoweza kufanikisha na kile ninachoweza kuthibitisha, ni kile ninachoamini kwamba Mungu amefanikisha kwa ajili yangu. Sina Shahada ya Sanaa, Ph.D., wala LL.D., mimi hata sina elimu ya shule ya msingi. Nisingeweza kufanikisha chochote, bali ninakubali kile Yeye alichofanikisha kwa ajili yangu pale Kalvari, wakati Kristo alipoyatoa maisha Yake kwa ajili yetu, na Mungu akamfufua kwenye siku ya ufufuo, kuthibitisha ya kwamba Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Ninakubali Mafanikio ya Mungu.

¹²⁶ Na ni njia ya Mungu iliyoandalika kwa ajili ya kila mtu aliye mgonjwa wa dhambi, ama mgonjwa wa kimwili, leo, ninawaomba mkubali Mafanikio ya Mungu. Na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu, kwa ajili ya maombi.

¹²⁷ Mungu Mtakatifu na wa Kiungu, tunakuja katika Uwepo Wako, tunaomba rehema, Bwana. Hatutamani, wala hatuna shauku ya haki. Tusingewenza kuistahimili haki ya Mungu, haki ya Mungu ingetuhukumu, na kutufanya wenyewe dhambi, na kutukatalia mbali.

¹²⁸ Hatuitamani sheria Yako, Baba, kwa sababu sheria Yako inatufanya sisi sote kuwa mwenye dhambi. Lakini tunatamani neema Yako, tunatamani neema Yako ya msamaha kupitia Yesu, Mwanaao, ambapo wote watakaoamini wanakubalika.

¹²⁹ Hatujaribu kuwazia chochote, Baba, kufanya mafanikio yoyote ya hakika, kutufanya shirika ama dhehebu. Hatujaribu kujifanya wakubwa, bali tunadumu tu wanyenyekevuna, kukushukuru Wewe kwa ajili ya Mafanikio ambayo umetufanya, kwa maana atakayejidhili atakwezwa; lakini ye ye ajikwezaye kwa mafanikio yake mwenyewe, bila shaka, atadhiliwa.

¹³⁰ Bariki kanisa hili dogo, Bwana, mchungaji wake wa thamani, hawa ndugu wa thamani walio pamoja nasi leo, mashemasi, wadhamini, hawa wanawake wa kupendeza, wasichana wadogo, na vijana wanaume wanaoketi hapa, kwenye hatua za mabadiliko ya maisha.

¹³¹ Mungu, tupe rehema Zako, tunayakubali Mafanikio Yako kupitia kwa Yesu. Tunaamini ya kwamba Yeye alikufa, naam, zaidi ya hayo, alifufuka tena siku ya tatu kwa ajili ya kuhesabiwa haki kwetu. Tunaamini ya kwamba Yeye alipaa juu, na hapo akamtuma Roho Mtakatifu apate kuwa Mwombezi na kutuongoza na kutuelekeza, Kristo katika umbo la Roho, ambaye angeishi ndani yetu na kufanya kazi zile zile ambazo Yesu alifanya kwa sababu ni Uzima Wake ndani yetu.

¹³² Ee Bwana, mahekalu yetu na yatakaswe, mioyo yetu isafishwe na kutokuamini kwote, nafsi zetu ziridhike na Kristo, Mafanikio Yako. Na jalia tuweze kuchukua rehema Yake na Neno Lake na kumleta Yeye halisi *sana* kwa watu hawa alasiri ya leo, kwamba maadamu kuna Grande Prairie, maadamu tu kuna watu hapa ambao wanaamini, wangali wanaamini, jalia hadithi hiyo isimuliwe, kwa sababu ya Uwepo Wake.

¹³³ Jalia lisababishe uamsho wa mtindo wa kale kuanza hapa ndani, watu wengi waokoke, kwa kuwa hii, labda, ni siku kuu ya kuzuriwa, wakati sote tumekusanyika pamoja kama watoto Wako waaminio. Tunaomba, katika Jina la Yesu, na kwa ajili Yake. Amina. 

61-0516M Njia Ya Mungu Iliyoandaliwa
Zion Gospel Tabernacle
Grande Prairie, Alberta Canada

SWAHILI

©2024 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org